

**N**ilizipokea kwa furaha taarifa za ajira mpya kutoka serikalini, kwani nami nilikuwa mmoja wa wanufaika. Nilipangiwa kuwa mwalimu kwenye shule ya sekondari Ikolonga iliyopo mkoani Simiyu.

Japokuwa Simiyu ni mbali kutoka nyumbani kwetu Kibakwe, Dodoma; hilo sikulijali. Nilinyoosha mikono mbinguni na kumshukuru Mwenyezi Mungu. Niliiona ajira kama upanga wa kuzichinjilia mbali shida zangu ambazo hadi wakati huo zilikuwa zimenifubaza mwili na roho. Hakika nilijiona mtu mpya; nikitoka katika hali ya 'kijitu' na kuwa 'mtu'.

Nilipowaarifu wazazi wangu juu ya jambo hilo walifurahi sana, naam, walifurahi zaidi yangu. Nahisi waliamini kuwa ningewapunguzia mzigo wa kunilea baada ya kukaa miezi mingi nyumbani bila ajira wala kazi yoyote yenye ujira unaoeleweka. Kukaa kwangu nyumbani bila kazi ilikuwa sawa na zigo la miiba kwao, japo walishindwa kunitua kwa kuwa mimi mtoto wao.

Mama alikuwa akinifanyia vitimbi ambavyo niliamini vilitokana na kukosa kwangu ajira. Kuna wakati niliporudi nyumbani, nilikuta chai haina sukari wala vitafunwa na nilipomuuliza aliishia kunijibu kwamba nitafute kazi nianze kujipatia mwenyewe hivyo vitu ninavyovihitaji. Nilipojitahidi kujitetea kwa kulalamikia ugumu wa kupata ajira, ndivyo alivyokuwa akiongea maneno makali ya kunirarua mtima. "Mtoto wa kiume acha uvivu na kulialia, kwani hao wote wenye kazi, wameajiriwa?" niliulizwa kwa kejeli.

Ukweli ni kwamba, nilitafuta sana kazi mjini, zinazohitaji kutumia nguvu na zile zenye kuhitaji akili, lakini jitihada zangu ziligonga mwamba. Hatimaye nilinyoosha mikono na kurudi kijijini kusubiri huruma ya serikali. Sasa kusema niache uvivu na kulialia, alimaanisha nini ilhali nilikwishamsimulia yote?

Manyanyaso na kunyanyapaliwa kwa kukosa ajira havikuishia nyumbani tu, hata mitaani hali ilikuwa hivyo. Kwa kuwa nilikuwa mmoja wa wasomi wachache pale kijijini na, wasomi wenzangu wote walikuwa wamekwishaajiriwa na walikuwa wakilipwa ujira mzuri, nilionekana kituko.

"Kasoma hadi chuo kikuu lakini amerudi kufugwa na wazee wake. Mitoto mingine ni hasara, heri lingefeli liishie kukata kuni za kupikia komoni kama wenzake. Kuna raha gani ya kusomesha kwa kujipinda halafu toto lije likae tu na mindevu yake, wewe ulilishe?"

"Wenzake wote wameoa isipokuwa yeye mhunimhuni tu!"

"Aoe ana cha kumlisha huyo mke na watoto?" Maneno haya niliyasikia siku moja nilipokuwa nikienda bombani kuteka maji. Niliwasikia akina mama wakisema bila kujua nilikuwa karibu. Nilihisi huenda mama alisimangwa na rafikize juu yangu kwa maneno kama hayo, ndiyo maana alianza kunifanyia vitimbi.

Vijana wa rika langu nao walikuwa wakinitenga na hawakutaka kunishirikisha kwenye kazi za kutumia nguvu wakidai mimi ni msomi hivyo

mambo yale nisingeyaweza. Wengine walinisihi niache tamaa kwani nisingeweza kufanya kazi zote peke yangu; zile za kisomi na zile za shambani. Sijui hawakuelewa kuwa sikuwa na ajira au walifanya hivyo kwa kunikomoa!

Niliumizwa sana na maisha hayo. Niliona thamani ya utu wangu ikishuka. Suala hilo lilinifanya muda mwingi nishinde makorongoni alimradi tu kukwepa mishale ya waja. Hivyo, nilipopata taarifa za ajira nilifurahi pasi na kifani.

\*\*\*

Baada ya ajira kutangazwa, nilipewa muda wa majuma mawili kwa ajili ya kujiandaa kabla ya kwenda kuripoti kwenye kituo cha kazi. Niliutumia muda ule kufanya maandalizi ya kutosha na kuwaaga ndugu, jamaa na marafiki. Nilitaka kumuonesha kila aliyenidharau kuwa utu wangu wa zamani umezikwa; ajira imenivika utu mpya.

Ili kuhakikisha taarifa ya kuajiriwa kwangu inafika kila pembe ya kijiji, nilienda kuomba ibada ya shukrani kanisani. Nililiasi kanisa kwa muda mrefu, lakini taarifa ile ya ajira ilinirejesha. Siku ya ibada ilitangazwa kanisani kuwa nimeajiriwa hivyo nimeenda kumshukuru Mungu na kumtolea sadaka. Watu walinipongeza hata wale ambao nilifahamu fika kuwa walikuwa wakinisimanga wakati nilipokuwa sina hili wala lile. Nami niliwashukuru kwa kejeli.

Mama naye aliacha kunifanyia vitimbi, badala yake akaanza kunijali na kunichangamkia. Wazazi wakanizawadia ng'ombe mmoja, siku ya gulio nilimuza na kupata fedha za kutosha kwa ajili ya maandalizi. Mama alinifungashia vitu kadha wa kadha kama vile mapazia na mashuka. Vilevile alinipikia mabumunda ya kula njiani siku ya safari.

Muda wa maandalizi ulipokwisha nilifunga safari kwenda katika kituo changu cha kazi...